# TCCIA INVESTMENT PLC

MKUTANO MKUU WA MWAKA
WA 14 WA WANAHISA 10/08/2019

DONDOO NA. 14/2/2019

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NNE UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 10 AGOSTI 2019 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO MAKUMBUSHO YA TAIFA, DAR-ES-SALAAM SAA TATU KAMILI (3.00) ASUBUHI.

Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 10 Agosti, 2019 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Makumbusho, Dar-es-Salaam. Mkutano utaanza saa Tatu kamili (3.00) asubuhi.

**Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne ni:**

14.1 Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne.

14.2 Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkuu wa Kumi na Nne.

14.3 Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2018.

14.4 Kupokea, kujadili na kuridhia Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2018.

14.5 Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018.

14.6 Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018.

14.7 Kupokea na kuridhia Pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Gawio kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018

14.8 Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la Bodi kuhusu Uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 31 Desemba, 2019 pamoja na Malipo yake.

14.9 Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi (Directors Fees).

14.10 Kupokea, kujadili na kuamua kuhusu Dondoo mbalimbali zitakazokuwa zimewasilishwa na wanahisa kabla ya tarehe 27 Julai, 2019.

14.11 Kufunga Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne.

Mwisho tunapenda kuchukua fursa hii kuwahimiza wanahisa kuhudhuria Mkutano huu muhimu.

**Angalizo:**

1. Mwanahisa atakayehudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne atatakiwa kujigharamia mwenyewe gharama za usafiri, malazi na chakula.

2. Mwanahisa anatakiwa aje na Cheti chake cha Hisa pamoja na kitambulisho chake, ambacho

ni aidha Kitambulisho cha Uraia, cha Mpiga Kura, Hati ya Kusafiria, Leseni ya Udereva au barua ya Utambulisho iliyotolewa na Mwenyekiti wa Mtaa anakoishi.

3. Mwanahisa anayestahili kuhudhuria Mkutano Mkuu na kupiga kura lakini akashindwa kuhudhuria kutokana na sababu mbalimbali anaweza kuwasilisha jina la Mbadala wake yaani “Proxy” ikiwa imeambatanishwa na Cheti cha Hisa na Kitambulisho cha Mwanahisa masaa 72 kabla ya siku ya Mkutano Mkuu. Fomu ya Proxy imeambatanishwa kwenye Taarifa hii.

4. Tunarudia na kusisitiza kuwa Dondoo za Wanahisa zitakazojadiliwa ni zile ambazo zitawasilishwa kabla ya tarehe 27 Julai, 2019 tu.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.

Donald J. Kamori

**Katibu**

Bodi ya Wakurugenzi

DONDOO NA. 14/3/2019

## KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TATU ULIOFANYIKA SIKU YA IJUMAA TAREHE 30 NOVEMBA, 2018 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KARIMJEE, KUANZIA SAA NNE NA DAKIKA ISHIRINI NA MBILI (4.22) ASUBUHI

**13.1 Mahudhurio**

Orodha ya Wajumbe pamoja na Wawakilishi wa Wanahisa waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu uliofanyika siku ya Ijumaa tarehe 30 Novemba, 2018 imeambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi. Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 1 na 2.

**13.2 Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 4.22 asubuhi baada ya Katibu kutangaza kuwa akidi inayohitajika imefikiwa.

**13.3 Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu**

Wajumbe walipokea, kujadili na hatimaye kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu.

**13.4 Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili**

Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili zilithibitishwa baada ya kufanya masahihisho yafuatayo:

Ukurasa wa 2 kifungu 12.3 neno Ndondoo lisomeke Dondoo.

**13.5 Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili**

Taarifa ilitolewa kuhusu utekelezaji wa maazimio mbalimbali yaliyopitishwa na Wajumbe wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili uliofanyika tarehe 10 Novemba, 2017. Mambo muhimu ambayo yalitolewa taarifa ni:

**13.5.1 Azimio la kuongeza Mtaji wa Kampuni na kuorodhesha Hisa za Kampuni kwenye Soko la Hisa la Dar-es-Salaam.**

Wajumbe walielezwa kuwa Azimio hili limetekelezwa na kwamba Hisa za Kampuni ziliorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar-es-Salaam tarehe 16 Machi, 2018.

**13.5.2 Azimio la kubadili jina la Kampuni**

Wajumbe walielezwa kuwa azimio limetekelezwa na kwamba tarehe 10 Mei, 2017, BRELA iliidhinisha jina jipya la Kampuni. Kuanzia tarehe hiyo Kampuni inajulikana kwa jina la TCCIA Investment Public Limited Company.

**13 .5.3 Azimio la Kuthamanisha Hisa za Kampuni**

Taarifa ilitolewa kuwa Azimio hili limetekelezwa na kwamba sasa hivi hisa moja ya zamani ni sawa na hisa 12.5.

**13.5.4 Azimio kuhusu Taarifa za kufanyika Mkutano Mkuu**

Taarifa ilitolewa kuwa Azimio hili limetekelezwa. Taarifa ya Mkutano ilitumwa siku 42 kabla ya tarehe ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu.

**13.4.5 Azimio kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi**

Taarifa ilitolewa kuwa Azimio hili limetekelezwa.

**13.4.6 Azimio kuhusu Uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Mwaka 2018**

Taarifa ilitolewa kuwa Azimio limetekeleza.

**13.4.7 Azimio kuhusu nafasi ya TCCIA kwenye Bodi ya Kampuni**

Taarifa ilitolewa kuwa azimio hili limetekelezwa.

**13.5 Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi kwa Mwaka 2017**

Wajumbe wa Mkutano Mkuu walielezwa kuwa Taarifa ya Bodi na Mahesabu ya Kampuni yaliyokaguliwa kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2017 zinaonyesha utendaji na shughuli za Kampuni.

Wajumbe walielezwa kuwa Mtaji wa Kampuni ulioidhinishwa (Authorised Share Capital) ni Shilingi 100,000,000,000. Wajumbe walieleza kwamba idadi ya hisa zote ni 5,000,000,000 kila moja ikiwa na thamani ya Shilingi 20. Hata hivyo, Wajumbe walielezwa Idadi ya hisa zilizolipiwa ni 71,092,400 ambazo zina thamani ya Shilingi 1,421,848,000. Pia Wajumbe waliarifiwa kuwa mpaka Desemba,31, 2017 Hisa za Kampuni zilikuwa hazijaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar-es-Salaam zikiwa na thamani ya Shilingi 250 kila moja.

Wajumbe walielezwa kuwa jukumu kubwa la Bodi ni kukuza na kuimarisha mtaji wake, kuongeza faida na thamani ya mtaji wake kwa kuwekeza kwenye sehemu zenye tija na manufaa. Wajumbe waliarifiwa, kuwa shughuli kuu za Kampuni ni kusimamia uwekezaji wake kwenye hisa za makampuni mbalimbali pamoja na kwenye dhamana za Serikali na amana za Mabenki.

**13.6 Wajumbe wa Bodi**

Taarifa ilitolewa kwamba kwa mwaka 2017 Wajumbe wa Bodi walikuwa kumi na moja (11). Wajumbe wote ni raia wa Tanzania na ni wenye sifa na uzoefu katika nyanja mbalimbali. Taarifa ilitolewa kuwa mwezi Julai, 2017, Ndugu Hanim A. Babiker aliyekuwa akiwakilisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (LAPF) kwenye Bodi kwa sasa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), alistaafu na nafasi yake kujazwa na Ndugu Peter W. Kifunguomali. Wajumbe walielezwa kwamba kama ilivyoagizwa wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Mbili taarifa imetolewa kuhusu idadi ya hisa zinazomilikiwa na kila Mjumbe wa Bodi.

### 13.7 Utawala kwenye Kampuni

Taarifa ilitolewa kuwa kwa mwaka 2017 Bodi ilifanya jumla ya vikao 9. Vikao vitano vilikuwa vya kawaida na vinne kwa ajili ya kujadili na kupitisha mambo muhimu. Ili kuhakikisha kuwa Bodi inatimiza wajibu wake ipasavyo kwa mwaka 2017, Bodi ilikuwa na Kamati mbili ambazo ni: Kamati ya Uwekezaji na Kamati ya Ukaguzi na Athari. Kamati ya Uwekezaji ilikuwa na jumla ya Wajumbe wanne. Kamati hii ilikutana mara nane kujadili taarifa za utendaji wa Kampuni. Kamati ya Ukaguzi na Athari ilikuwa na Wajumbe watatu na ilikutana mara sita kujadili taarifa za Ukaguzi za kila Robo Mwaka zinazoandaliwa na Mkaguzi wa Mahesabu wa Ndani.

### 13.8 Shughuli ambazo zilifanywa na Bodi

Taarifa ilitolewa kuwa pamoja na kusimamia shughuli za Kampuni kwa mwaka 2017 Bodi ilitekeleza shughuli zifuatazo:

- Kusimamia zoezi la kuuza hisa za Kampuni lililofanyika mwezi Februari/Machi 2017.
- Kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Kampuni na Mpango wa Biashara wa Mwaka.
- Kuandaa Kanuni za Bodi (Board Charter).
- Kupokea na kujadili taarifa za Mkaguzi wa Ndani wa Mahesabu yanayowasilishwa kila robo mwaka.
- Kupokea na kujadili taarifa za utendaji zinazoaandaliwa na Menejimenti kwa kila robo mwaka.
- Bodi ilipitia na kuidhinisha marekebisho ya Sera ya Kampuni kuhusu Uwekezaji.
- Kupanua wigo wa Uwekezaji kwa lengo la kupunguza athari zinazoweza kutokea kwa kutegemea chazo kimoja, hususani malipo ya gawio.

### 13.9 Malipo ya Gawio

Bodi ilipendekeza kuwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2017 malipo ya gawio yawe sawa na Shilingi 2.54 kwa kila hisa moja. Hii ni sawa na asilimia 75 ya faida iliyopatikana baada ya kutenga fungu la kodi. Kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kiasi kitakachobaki kitatumika kuimarisha mtaji wa Kampuni.

### 13.10 Mipango ya Baadae

Taarifa ilitolewa kuwa kutokana na mwenendo wa Soko la Hisa la Dar-es-Salaam kutokuwa mzuri, Bodi imeamua kuchukua hatua ya kupanua wigo wa uwekezaji badala ya kutegemea mapato ya gawio kutoka makampuni tulikowekeza. Kwa hiyo Kampuni imeanza kuwekeza kwenye Dhamana za muda mrefu za Serikali na Makampuni ambazo zinalipa riba nzuri na pia kwenye amana za Mabenki.

### 13.11 Uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu kwa mwaka 2018

Taarifa ilitolewa kuwa Kifungu Namba 10 cha Katiba ya Kampuni kinatamka kwamba Wakati wa Mkutano Mkuu wa kila mwaka Wajumbe watateua Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni ambaye

atahudumu mpaka Mkutano Mkuu utakapofanyika tena. Mkutano Mkuu ulielezwa kwamba Kampuni ya Ukaguzi na Ushauri ya BACCON, Certified Public Accountants, ndiyo iliyokagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka 2017. Kampuni ilianza kukagua Mahesabu ya Kampuni mwaka 2013. Tangu wakati huo Kampuni hii imekuwa ikikagua Mahesabu ya Kampuni kila mwaka baada ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kampuni. Bodi imekuwa ikiridhika na utendaji kazi wake tangu ilipoanza kukagua Mahesabu ya Kampuni. Hata hivyo, kwa mwaka 2018, Bodi ilitafakari kwa kina suala hili na kuamua kuwa kwa mwaka 2018 makampuni mengine pamoja na BACCON yakaribishwe kushiriki katika zabuni na kwamba maombi yafanyiwe tathimini kwa kuzingatia uwezo kitaaluma, uzoefu na gharama. Jumla ya Makampuni sita yalialikwa lakini ni makampuni matatu tu ndiyo yaliyowasilisha maombi. Makampuni hayo ni:

- BACCON Certified Public Accountants.
- BM Associates.
- CROWE Tanzania Limited.

Baada ya kufanyiwa tathmini, Bodi iliamua kupendekeza kwa Mkutano Mkuu kuwa Kampuni ya CROWE Tanzania Limited iteuliwe kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka 2018 kwa gharama ya Shilingi 16,402,000 pamoja na VAT.

Mwisho Wajumbe waliombwa kupokea, kujadili na kuidhinisha Kampuni ya Ukaguzi na Ushauri ya CROWE Tanzania Limited kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka 2018 kwa gharama ya Shilingi 16,402,000 pamoja na VAT.

### 13.12 Malipo ya Wakurugenzi (Directors Fees)

Taarifa ilitolewa kuwa Malipo ya Wakurugenzi wa Bodi (Directors Fees) yameanishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 kinatamka kuwa: "The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in a General Meeting". Mkutano Mkuu ulielezwa kwamba kwa mwaka 2017 Wajumbe wanaombwa kupokea, kujadili na kuidhinisha malipo ya Wakurugenzi kiasi cha Shilingi 4,000,000 kwa kila Mkurugenzi. Pia Wajumbe walielezwa kuwa kiasi kinachopendekezwa na Bodi ni sawa na kilicholipwa mwaka 2016.

### 13.13 Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni yaliyokaguliwa kwa mwaka wa 2017

Wajumbe walielezwa kuwa kwa mwaka 2017 Kampuni iliendelea kufanya vizuri. Mapato ya Kampuni yaliongezeka kutoka Shilingi 1,086.6 mwaka 2016 na kufikia Shilingi 1426.7 milioni. Hili ni ongezeko la asilimia 31.3. Matumizi yaliongezeka kwa asilimia 24 kufikia Shilingi 1074.5. Ilielezwa kwamba ongezeko katika matumizi ilitokana na gharama za uendeshaji na pia malipo ya gharama za Wakili (Legal fees). Faida baada ya kutenga fungu la kodi ilikuwa sawa na Shilingi 246.57 milioni ikilinganishwa na faida ya Shilingi 154.17 milioni kwa mwaka 2016. Kwa mwaka 2017 thamani ya hisa zinazomilikiwa na Kampuni iliongezeka kwa Shilingi 2,726.44 milioni. Mtaji wa Kampuni pia uliongezeka kutoka Shilingi 27,805.92 milioni mwaka 2016 kufikia Shilingi 30,379.26 milioni.

### 13.14 Uhai wa Kampuni

Mwisho Mkutano Mkuu ulielezwa kuwa taarifa ya fedha inatoa mtazamo wa hali halisi kuhusu

mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2017. Bodi inaridhika kwamba mpaka sasa hakuna sababu yeyote inayoonyesha kuwa Kampuni haitaendelea kufanya vizuri kwa miezi mingine 12 kuanzia kutolewa kwa taarifa hii.

### 13.15 Majadiliano

Wajumbe walipokea na kujadili mada mbalimbali zilizowasiliishwa na Bodi mbele ya Mkutano Mkuu.

a) Taarifa ya Mahesabu

Wajumbe wa Mkutano Mkuu walipokea na kujadili Tarifa ya Mahesabu ya Kampuni yaliyokaguliwa kwa mwaka 2017 na kushauri kuwa Bodi ichukue hatua zitakazowezesha Kampuni kuongeza mapato na pia kubana matumizi. Walisisitiziza kuwa kuna haja ya kupunguza ukubwa wa Bodi na idadi ya vikao vinavyofanyika.

b) Malipo ya Gawio

Wajumbe walipokea na kujadili pendekezo la Bodi la kulipa gawio la Shilingi 2.54 kwa kila hisa moja na kuazimia kwamba kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2017 Kampuni ilipe gawio la Shilingi 2.54 kwa kila hisa moja na kwamba gawio lilipwe siku 90 baada ya azimio hili.

c) Malipo ya Wakurugenzi wa Bodi

Kuhusu Malipo ya Wakurugenzi, Wajumbe walijadili na kuazimia kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi 4,000,000 kila mmoja.

d) Uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu kwa Mwaka 2018

Wajumbe walipokea na kujadili pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu kwa mwaka 2018. Baadhi ya Wajumbe walieleza kuwa kwa vile Kampuni ya BACCON imekuwa ikifanya kazi yake vizuri kwa kipindi chote inastahili kuendelea. Hata hivyo baada ya majadiliano, Mkutano Mkuu uliamua kuazimia kwamba CROWE Tanzania Limited wateuliwe kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha unaoishia Desemba 31, 2018 kwa gharama ya Shilingi 16,402,000 kama ilivyopendekezwa na Bodi.

### 13.16 Madai ya Dkt. Gideon H. Kaunda dhidi ya Kampuni

Mwenyekiti alitoa taarifa fupi kuhusu madai dhidi ya Kampuni kutoka kwa Dkt Kaunda aliyekuwa akitaka alipwe fidia ambayo aliita Equitable Compensation kutokana na Hati ya nyumba yake iliyotumika kwa ajili ya mkopo wa US $150,000 ambao ulitolewa na Benki ya Azania kwa Kampuni ili kuiwezesha kushiriki katika Zabuni ya kununua asilimia 49 ya hisa za NMB ambazo Serikali iliamua kuziuza kwa wawekezaji waliojiunga katika makundi (Consortium Groups).

Mkutano Mkuu uliarifiwa kuwa Bodi ilikataa madai hayo na iliamua kutafuta ushauri wa kisheria na Mwanasheria na akapendekeza madai yake yapelekwe kwenye Jopo la Usuluhishi. Wajumbe waliarifiwa kuwa Wasuluhishi hao walishindwa kukubaliana na hivyo Dkt. Kaunda aliamua kupeleka suala hili mbele ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ambao walishauri kuwa mgogoro huo utatuliwe kwa njia ya usuluhishi.

Wajumbe waliarifiwa, baada ya vikao kadhaa vya usuluhishi, Jopo lilitoa taarifa yake ambapo madai yake ya msingi yalikataliwa. Mwisho Jopo liliamua kutoa Tuzo ya Sh. 450.0 milioni na riba ya asilimia 7 kwa mwaka na malipo ya gharama za kuendesha kesi kiasi cha shilingi 100 milioni. Bodi haikuridhika na uamuzi huo, na kuamua kuomba Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara kutengua uamuzi wa Jopo la Usuluhishi. Mwenyekiti alimaliza kwa kuwaeleza Wajumbe wa Mkutano kuwa; suala hili kwa sasa liko Mahakamani hakutakuwa na mjadala wowote. Wanahisa mtajulishwa uamuzi wa Mahakama utakapotoka.
Hata hivyo kabla ya Mkutano Mkuu kufungwa Afisa Mtendaji Mkuu aliwatangazia Wajumbe kuwa, Mahakama Kuu imetoa uamuzi wake na kwamba Mahakama imetengua Tuzo iliyotolewa na Jopo la Usuhishi na kwamba Rufaa ya Bodi imekubaliwa.

### 13.17 Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi

Kabla ya kuanza mchakato wa Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi, Mkutano Mkuu ulichagua Msimamizi wa Uchaguzi na Msaidizi wake. Waliochaguliwa ni:

- Ndugu Jackson Tairi Nyakuyeya - Mwenyekiti
- Ndugu Gaudensia Kaliba Tungaraza - Makamu Mwenyekiti

Wajumbe wa Mkutano Mkuu walielezwa baada ya Azimio la kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi lilopitishwa na Mkutano Mkuu wa 13 kutoka 12 mpaka 7, utaratibu wa uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi utakuwa kama ifuatavyo:

- LAPF itatengewa nafasi mbili (2).
- TCCIA itatengewa nafasi moja (1).
- Mjumbe mmoja atachaguliwa kutoka kundi la Wanataaluma. Mjumbe huyo atapigiwa kura na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu.
- Wajumbe watatu wenye sifa zinazotakiwa watachaguliwa na Wanahisa wadogo na kwamba LAPF na TCCIA hawatashiriki katika zoezi la kupiga kura.

Vile vile Wajumbe walielezwa kwa kina sifa zinazotakiwa na pia hatua zilizochukuliwa, ikiwa ni pamoja na kutangaza nafasi kwenye magazeti, kumtumia Mtalaam wa Rasilimali Watu kufanya tathimini ya maombi na kuwasilisha mapendekezo yake. Mwisho Mkutano Mkuu uliombwa kuridhia mambo yafuatayo:

- Kuridhia orodha ya wanahisa waliomba kuchaguliwa kuwa Wajumbe wa Bodi kwa kipindi cha miaka mitatu.
- Kupokea na kuridhia Wajumbe wawili walioteuliwa na LAPF.
- Kupokea na kuridhia uteuzi wa Rais wa Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo kuwa Mjumbe wa Bodi.
- Kumpigia kura Mjumbe mmoja ambaye yuko kwenye kundi la Wataalam na baada ya hapo kuchagua Wajumbe watatu.

- Wakati wa kupiga kura kila hisa moja ni sawa na kura moja.

Wajumbe waliopigiwa kura na idadi ya kura walizopata kama ilivyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi imeonyeshwa hapo chini.

Uchaguzi wa Mjumbe mmoja kutoka Kundi la Wataalam

| Jina la Mgombea | Idadi ya Kura alizopata | Asilimia ya Kura zilizopigwa |
|---|---|---|
| Ndg. Nathan Mnyawami | 28,214,812 | 64.07 |
| Ndg Joseph Kahungwa | 8,169,617 | 18.55 |
| Dkt. Gideon Kaunda | 5,518,346 | 12.53 |
| Prof. Lucian Msambichaka | 1,329,772 | 3.02 |
| Ndg. Arphaxad Masambu | 731,938 | 1.66 |
| Ndg. Julius Kaijage | 36,738 | 0.08 |
| Ndg. Magdalene Mkocha | 22,547 | 0.05 |
| Ndg. Nathaniel Mbwambo | 10,687 | 0.02 |

Kulingana na matokeo ya kura ambazo kila Mgombea alipata Msimamizi wa Uchaguzi alimtangaza **Ndugu Nathan Mnyawami** kuwa Mshindi katika Kundi la Wataaluma.

Baada ya hapo Wajumbe walipiga kura kuchagua Wajumbe watatu (3) wa Bodi.

**Matokeo ya Uchaguzi wa Wajumbe watatu (3)**

| | | |
|---|---|---|
| Prof. Lucian Msambichaka | 12,943,458 | 28.07 |
| Ndugu Joseph Kahungwa | 9,118,574 | 19.78 |
| Ndugu Magdalene Mkocha | 7,603,014 | 16.49 |
| Dkt. Gideon Kaunda | 6,165,046 | 13.37 |
| Ndugu Arphaxad Masambu | 6,136,094 | 13.31 |
| Ndg. Nathaniel Mbwambo | 3,621,011 | 7.85 |
| Ndugu Julius Kaijage | 510,783 | 1.11 |
| Ndugu Ranald Kato | 3,450 | 0.01 |
| Ndugu Godfrey Pasape | 3,200 | 0.01 |
| Lt. (Rtd) Maganga Sengelema | 100 | 0.00 |

Baada ya kura kuhesabiwa, kwa kuzingatia Idadi ya kura alizopata kila Mgombea kama inavyoonyeshwa hapo juu Msimamizi wa Uchaguzi alitangaza kuwa wafuatao ndio walioshinda

**Prof. Lucian Msambichaka**

**Bwn. Joseph Kahungwa**

**Bi. Magdalene Mkocha**

**Kufunga Mkutano**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa Majadiliano ya kina ambayo lengo lake ni kuimarisha shughuli za Kampuni. Aliwahakikishia wajumbe kwamba bado itachukua hatua kutekeleza mambo yote yaliyoamuliwa na Mkutano Mkuu. Mwisho aliwashukuru Wajumbe kwa kushiriki katika kuchagua Bodi Mpya na kufunga Mkutano saa 11.10 jioni.

__________________________ ______________________

| | |
|---|---|
| Ndg. Fortunatus Magambo | Donald J. Kamori |
| **Mwenyekiti** | **Katibu** |

Tarehe________________

## ORODHA YA WALIOUDHURIA MKUTANO MKUU ULIOPITA

| CDS No. | Shareholder Name | Rep Type | Shares | % Shares |
|---|---|---|---|---|
| 51121 | THE LOCAL AUTHORITIES PENSIONS FUND | Proxy | 28,100,300 | 38.45 |
| 569364 | MKOMBOZI FISHING & MARING TRANSPORT LTD | Proxy | 4,215,000 | 5.77 |
| 569351 | ABBASI EXPORTS LTD | Proxy | 1,686,000 | 2.31 |
| 150344 | CHRISTOPHER MWITA GACHUMA | Proxy | 1,405,000 | 1.92 |
| 121481 | FAYAZ FEROZ RASHID | Proxy | 1,236,400 | 1.69 |
| 46802 | NIMROD ELIREHEEMAH MKONO | Proxy | 1,123,975 | 1.54 |
| 149308 | ELVIS ARISTABLUS MUSIBA | Proxy | 674,375 | 0.92 |
| 569116 | JAMES MAJUKANO GEGE | Proxy | 561,975 | 0.77 |
| 105271 | LUCIAN AMBROSE MSAMBICHAKA | Self | 464,200 | 0.64 |
| 569290 | ABIHUDI SAULO MHIDZE | Proxy | 393,387 | 0.54 |
| 569296 | PROF.BURTON LUNOGELO MHAMILAWA MWAMILA | Proxy | 337,200 | 0.46 |
| 142685 | NATHANIEL RAJABU MBWAMBO | Self | 303,462 | 0.42 |
| 122664 | CHARLES JOSEPH MWAPINGA | Proxy | 281,000 | 0.38 |
| 154513 | JONATHAN SHAURI KARAZE | Self | 281,000 | 0.38 |
| 569170 | JANE ROBERT MASABARI | Proxy | 281,000 | 0.38 |
| 569356 | TESE & TECHE ENGINEERING LTD | Proxy | 252,900 | 0.35 |
| 569210 | ALOIS JOSEPH MWAMANGA | Proxy | 231,975 | 0.32 |
| 569301 | AMRAN KHERI BATENGA | Proxy | 224,800 | 0.31 |
| 569202 | DR.STERGOMENA LAWRENCE TAX | Proxy | 168,600 | 0.23 |
| 83945 | FRANK TIMOTH MSUYA | Proxy | 168,575 | 0.23 |
| 105803 | OSCAR NICHOLAUS QUIYENGA | Self | 140,500 | 0.19 |
| 569327 | TCCIA HQ | Proxy | 120,125 | 0.16 |
| 569640 | ENOCK DANIEL MASANJA | Self | 119,383 | 0.16 |
| 569537 | BENNY RUMISHAELI MAKUNDI | Proxy | 112,400 | 0.15 |
| 569265 | DR. GIDEON HOSEA KAUNDA | Self | 112,400 | 0.15 |
| 124080 | MAGDALENA NELSON ENOCK MKOCHA | Self | 100,562 | 0.14 |
| 569813 | GERALD FONGA MATEMU | Self | 73,400 | 0.10 |
| 569147 | HAMAD JUMBE MENYE | Self | 73,050 | 0.10 |
| 569696 | COSMAS MORIS HONERA | Self | 70,250 | 0.10 |
| 211897 | EMMANUEL OSWALD MSAMBICHAKA | Proxy | 66,513 | 0.09 |
| 569335 | TCCIA MWANZA | Proxy | 61,825 | 0.08 |
| 569287 | INTERMECH ENG./P.CHISAWILLO | Proxy | 60,413 | 0.08 |
| 569251 | MSANGI MABIRANGA TSETONGA | Self | 56,200 | 0.08 |
| 143915 | ABED AFWILILE MWASAJONE | Self | 56,200 | 0.08 |
| 129912 | PHYLLIS MARY JAMES | Self | 56,200 | 0.08 |
| 569338 | TCCIA TANGA | Proxy | 56,200 | 0.08 |
| 569279 | DR.VICENT ISAAC MHADA | Proxy | 56,200 | 0.08 |
| 569902 | GEORGE CHRISTOACHILIA SAM | Proxy | 56,200 | 0.08 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 569325 | TCCIA DAR ES SALAAM | Proxy | 56,200 | 0.08 |
| 569907 | MOHAMED BURHAN | Proxy | 56,200 | 0.08 |
| 569102 | ADOLPH MICHAEL SHOKI | Proxy | 49,150 | 0.07 |
| 569326 | TCCIA DODOMA | Proxy | 44,962 | 0.06 |
| 212421 | KUHUNGA PATRICK MSAMBICHAKA | Proxy | 42,150 | 0.06 |
| 569359 | KADOLO INVESTIMENT CO. LTD | Proxy | 39,338 | 0.05 |
| 569320 | CHAMA CHA WALIMU WASTAAFU | Proxy | 33,725 | 0.05 |
| 98946 | SALEEM AKBER PARPIA | Proxy | 30,900 | 0.04 |
| 108903 | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | Self | 28,100 | 0.04 |
| 162321 | GAUDENSIA KALIMBA TUNGARAZA | Self | 28,100 | 0.04 |
| 569334 | TCCIA MTWARA | Proxy | 28,100 | 0.04 |
| 569675 | YAKUB AYUBU HASHAM | Proxy | 28,100 | 0.04 |
| 569337 | TCCIA SHINYANGA | Proxy | 28,100 | 0.04 |
| 569670 | JANE NKULANGOWE AGWANDA | Proxy | 28,100 | 0.04 |
| 569332 | TCCIA MBEYA | Proxy | 28,100 | 0.04 |
| 47297 | LEONARD AUGUSTINO SANGA | Proxy | 25,275 | 0.03 |
| 546814 | AMINA ATHUMANI FUPY | Proxy | 25,000 | 0.03 |
| 519601 | MARLEY RASHID DIGAGA | Self | 25,000 | 0.03 |
| 107592 | NATHAN EDWARD MNYAWAMI | Self | 19,675 | 0.03 |
| 163196 | KUKA MERERE MWANGANYA | Self | 19,675 | 0.03 |
| 70522 | ELIFASI ELINIMO MSWIA | Self | 16,863 | 0.02 |
| 569559 | JULIUS MUTABUZI KAIJAGE | Self | 16,863 | 0.02 |
| 546522 | SCHOLASTIKA JAPHET HASUNGA | Self | 15,000 | 0.02 |
| 569184 | JOEL TIMOTH CHIKOMA | Self | 14,613 | 0.02 |
| 569284 | SHIJA PAUL MTALIS | Self | 14,050 | 0.02 |
| 569196 | GUSTAV CONRAD LAULAU | Self | 14,050 | 0.02 |
| 557064 | ERNEST THOMAS MSIGWA | Proxy | 14,050 | 0.02 |
| 569226 | FATUMA ABDALLAH KATUNZI | Self | 14,050 | 0.02 |
| 570017 | ERICA MBURU KIGALU | Proxy | 14,050 | 0.02 |
| 570023 | ISHMAEL LAISER | Self | 14,050 | 0.02 |
| 569341 | TCCIA COAST | Proxy | 14,050 | 0.02 |
| 569389 | MARY NEEMA MSIGWA | Proxy | 14,050 | 0.02 |
| 569336 | TCCIA RUKWA | Proxy | 14,050 | 0.02 |
| 569331 | TCCIA LINDI | Proxy | 14,050 | 0.02 |
| 99653 | JUSTINO SIMBA JEKELA | Proxy | 14,050 | 0.02 |
| 130174 | IMELDA CELESTINE BULYOTA | Proxy | 12,500 | 0.02 |
| 514523 | DONALD JIMOGI KAMORI | Self | 12,500 | 0.02 |
| 546726 | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | Self | 12,500 | 0.02 |
| 219736 | DONALD JIMOGI KAMORI | Self | 11,238 | 0.02 |
| 569139 | JOYCE KIUNSI BENJAMINI | Proxy | 11,238 | 0.02 |
| 569733 | MATONDO NONI SAYENDA P. | Proxy | 11,237 | 0.02 |
| 515900 | JOAN JAMES MNGODO | Self | 10,000 | 0.01 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 123952 | NEEMA MSENGI MASAMBU | Proxy | 10,000 | 0.01 |
| 569168 | KENNEDY NELSON SIMUNDI | Self | 9,985 | 0.01 |
| 569463 | ALPHONCE TLUWAY PANGA | Self | 8,437 | 0.01 |
| 569578 | GODFREY MDACHI HIZA | Proxy | 8,425 | 0.01 |
| 569437 | MARY MEINULF NDIMBO | Proxy | 7,812 | 0.01 |
| 165266 | JUMANNE HAJI MANGARA | Self | 7,378 | 0.01 |
| 569374 | MHEGA INVESTIMENT | Proxy | 7,300 | 0.01 |
| 569211 | MAYASSA MOHAMED SHARIF MUBAGO | Self | 7,025 | 0.01 |
| 569672 | HILDA KOKULAMUKA TEGAMAISHO | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 569757 | KULSUMBAI HUSSEIN MANJI | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 569760 | MOHAMEDMOHSI HUSSEIN MANJI | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 570137 | ALEMAN HUSSEIN MANJI | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 570235 | KUMAYL HUSSEIN MANJI | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 570212 | JAWAD HUSSEIN MANJI | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 569207 | MOHAMED KASSIM KIMBEWELE | Self | 5,625 | 0.01 |
| 569329 | TCCIA KIGOMA | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 569482 | AVELINA LUKELO DANDA | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 569436 | MWANAHAMISI RAMADHANI KITIVO | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 569803 | ISHMAEL SAGIRAKI LAISER | Self | 5,625 | 0.01 |
| 569598 | JACKSON TAIRI NYAKUYEYA | Self | 5,625 | 0.01 |
| 569758 | SUKAINA HUSSEIN MANJI | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 569759 | HUSSEIN MANJI PIRBHAI | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 205322 | ADELINA SIMEON MBONIMANA | Self | 5,625 | 0.01 |
| 46261 | CHARLES AWEDA GORANGA | Self | 5,625 | 0.01 |
| 40472 | PATRICK ZALLI MAPONGO | Self | 5,625 | 0.01 |
| 178989 | ALLY MOHAMED MBILIKIRA | Self | 5,625 | 0.01 |
| 569727 | ZUHURA MURSALI MSAMBACHI | Self | 5,625 | 0.01 |
| 570207 | JACQUELINE NGOMUO | Self | 5,625 | 0.01 |
| 569206 | DR.TUMAINI EDWARD MHADA | Proxy | 5,625 | 0.01 |
| 88062 | SYNPHOROSE EVARIST BAITWA | Self | 5,000 | 0.01 |
| 524051 | ELIBARIKI AIWEDA MBOYA | Self | 5,000 | 0.01 |
| 504917 | ISRAEL EMMANUEL KINGU | Self | 5,000 | 0.01 |
| 570337 | KHADIJA HASSAN CHAGULILO | Self | 5,000 | 0.01 |
| 570338 | RUKIA MAKARANGA | Proxy | 5,000 | 0.01 |
| 569288 | REHEMA AHMAD NGATANDA | Self | 4,775 | 0.01 |
| 569411 | MENAS MARKO LIKUKU | Self | 4,775 | 0.01 |
| 569656 | SHAMTE SEIFU NGURANGWA | Self | 4,212 | 0.01 |
| 569197 | EDGAR JOEL KAHABWA | Self | 4,163 | 0.01 |
| 123944 | NEEMA M. MASAMBU DGAGOMAS ARPHAXAD MASAMBU | Proxy | 4,000 | 0.01 |
| 39657 | BENNY RUMISHAEL MAKUNDI | Proxy | 4,000 | 0.01 |
| 136787 | ARPHAXAD G. A. MASAMBU | Proxy | 4,000 | 0.01 |
| 249920 | AGRIPINA ISRAEL MWIYOLA | Proxy | 3,592 | 0.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 570377 | PHILIPO TELETELA | Proxy | 3,375 | 0.00 |
| 569430 | ALFRED SALUM NDEGIPARA | Proxy | 3,375 | 0.00 |
| 546547 | JOEL MABULA SHIMBA | Self | 3,300 | 0.00 |
| 546334 | DANIEL DAUD UMBUH | Proxy | 3,000 | 0.00 |
| 546457 | TANGAMANO SACCOS LTD | Proxy | 3,000 | 0.00 |
| 123946 | NEEMA M. MASAMBU | Proxy | 3,000 | 0.00 |
| 123945 | NEEMA M. MASAMBU | Proxy | 3,000 | 0.00 |
| 162115 | ATHUMANI RAMADHANI ATHUMAN | Self | 3,000 | 0.00 |
| 569182 | MATILDA MEINUS NDIMBO | Self | 2,813 | 0.00 |
| 569536 | ABILAHI SALUMU CHINDOLO | Proxy | 2,813 | 0.00 |
| 570495 | HAPPY PAULO MWETA | Self | 2,813 | 0.00 |
| 569426 | LATIFA ERNEST KISANJI | Self | 2,813 | 0.00 |
| 569575 | HASHIM BAKARI SHEKILINDI | Self | 2,813 | 0.00 |
| 570464 | DIDACUS MWITA NDEMERA | Self | 2,813 | 0.00 |
| 569660 | SABINA CYPRIAN MALAMBELA | Self | 2,812 | 0.00 |
| 569632 | STEVEN SABHI MWITA | Self | 2,812 | 0.00 |
| 569577 | MOKORO MAGUYE TENYAROCHE | Self | 2,812 | 0.00 |
| 569633 | SAMWEL SYLVESTA LAYDER | Self | 2,812 | 0.00 |
| 569620 | BENARD FRANCIS LENYUNGU | Self | 2,812 | 0.00 |
| 570650 | PENIEL SHILEKIREMUU MWASHA | Self | 2,812 | 0.00 |
| 569383 | PACRASE HAYSHIT BURA | Proxy | 2,812 | 0.00 |
| 569835 | SAID ISSA LITANDA | Proxy | 2,812 | 0.00 |
| 569425 | MSAFIRI ROGEGA MONGATEKO | Proxy | 2,812 | 0.00 |
| 140920 | MUHOCHI RAPHAEL MARWA | Self | 2,812 | 0.00 |
| 46683 | KEBRON ANDERSON MAHOO | Self | 2,500 | 0.00 |
| 132624 | JEREMIA JAPHET MUNA | Self | 2,500 | 0.00 |
| 209979 | MARY KENNETH KAZENGA | Self | 2,000 | 0.00 |
| 546458 | NEMES JOSEPH KIAMA | Self | 2,000 | 0.00 |
| 528500 | GEORGE KIANGO LYIMO | Proxy | 2,000 | 0.00 |
| 569440 | MARIAM HUSSEIN MLONJA | Self | 1,850 | 0.00 |
| 154685 | KASA SAIDI MLONJA | Proxy | 1,638 | 0.00 |
| 176385 | AYOUB MBWANA MTAWAZO | Self | 1,512 | 0.00 |
| 510580 | EVA EUSTACK TARIMO AND/OR STANLEY KAMOTE | Self | 1,500 | 0.00 |
| 437763 | MJAHIDI B KAMUGISHA | Proxy | 1,500 | 0.00 |
| 569431 | HUSSEIN LILLA MLONJA | Proxy | 1,500 | 0.00 |
| 546553 | SCOLASTIKA MOHAMED NZIKU | Self | 1,500 | 0.00 |
| 571093 | YOHANA GABJOJIKA GILAP | Self | 1,400 | 0.00 |
| 569298 | SALEHE ABDALLAH BAHAJ | Self | 1,400 | 0.00 |
| 570774 | ABDALLAH ALLY BAHAJ | Proxy | 1,400 | 0.00 |
| 570786 | ALLY ABDALLAH BAHAJ | Self | 1,400 | 0.00 |
| 570956 | MARIAM SALEH BENESHAO | Proxy | 1,400 | 0.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 569264 | GODLAINESS AINAENY MAEDA | Self | 1,400 | 0.00 |
| 569109 | UNDUGU TIE & DIE | Self | 1,400 | 0.00 |
| 569443 | ALEX PACRAS RWEYEMAMU | Self | 1,400 | 0.00 |
| 569330 | TCCIA - KILOMBERO | Proxy | 1,400 | 0.00 |
| 569592 | HASHIM HAJI OLOTU MATINGA | Self | 1,400 | 0.00 |
| 569698 | DONALD NZAGA WARIOBA | Self | 1,400 | 0.00 |
| 569485 | SIXTUS THADEUS KAKUNDA CHAILA | Self | 1,400 | 0.00 |
| 569557 | SALEHE SHOMARI MBANA | Self | 1,400 | 0.00 |
| 569260 | ANWAR ABDALLAH BAHAJ | Self | 1,400 | 0.00 |
| 155250 | MARIETHA ALEX NDIMBO | Proxy | 1,400 | 0.00 |
| 118471 | MEINULF RAPHAEL NDIMBO | Proxy | 1,400 | 0.00 |
| 152707 | BENJAMIN CHRISPIN MAKOLE | Self | 1,400 | 0.00 |
| 153898 | SUDI ATHUMANI KIHAMAYA | Proxy | 1,400 | 0.00 |
| 569645 | CHIKU HUSSEIN MLONJA | Proxy | 1,375 | 0.00 |
| 569307 | ABDALLAH HUSSEIN MLONJA | Self | 1,250 | 0.00 |
| 537753 | CORONERY SERIKALI KASESA | Self | 1,250 | 0.00 |
| 546440 | MARIA LUCIAN MDENDEMI | Self | 1,200 | 0.00 |
| 546464 | GILBERT BURCHARD BAISI | Self | 1,000 | 0.00 |
| 514860 | RAMADHANI SALUM CHAMBUSO | Self | 1,000 | 0.00 |
| 546248 | JAMILA DAUD KHATAN | Self | 1,000 | 0.00 |
| 546502 | MELIACK MOSSES MOLLEL | Self | 800 | 0.00 |
| 546497 | JOSEPH AUGUSTINE MTUY | Proxy | 750 | 0.00 |
| 546807 | STEPHEN GERVAS KARUGILA | Self | 750 | 0.00 |
| 553220 | SUSAN DANIEL NASSORO | Self | 700 | 0.00 |
| 546371 | SABINUS THOMAS HAULE | Self | 600 | 0.00 |
| 544949 | WINFRIDA ELIAB CHIDUO | Self | 600 | 0.00 |
| 546425 | HILDA KOKULAMUKA TEGAMAISHO | Proxy | 550 | 0.00 |
| 514974 | PILLY VITALIS ALLY | Proxy | 500 | 0.00 |
| 546241 | PETER RUDAGUZA SEMUGURUKA | Self | 500 | 0.00 |
| 546423 | NDYABULU RASHID KAYUGWA | Self | 500 | 0.00 |
| 546468 | WILLIAM MATAI MWAKALUNDWA | Self | 500 | 0.00 |
| 546791 | MHEGA INVESTMENT | Proxy | 500 | 0.00 |
| 546548 | JUMA BILAL MLENDELA | Self | 500 | 0.00 |
| 546491 | EDITH HERBERT MALANGALILA | Self | 500 | 0.00 |
| 51921 | IBRAHIM MASUDI NZOWAH | Self | 500 | 0.00 |
| 55653 | HERRY MEINRAD KIWAYA | Self | 500 | 0.00 |
| 80125 | ANDREW YUSTIN KAHESA | Self | 500 | 0.00 |
| 140055 | PERPETUA PATRICK MBATTA | Self | 500 | 0.00 |
| 546276 | EMMANUEL EUSTACE ISHASI | Proxy | 400 | 0.00 |
| 546609 | RENATUS EMMANUEL RUGEMALIRA | Self | 400 | 0.00 |
| 514881 | HASSAN YUSSUF TIPA | Self | 375 | 0.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 546427 | PAUL MANGWENA KIHENGU | Proxy | 350 | 0.00 |
| 569648 | PILLY FADHILI MWESA | Proxy | 312 | 0.00 |
| 546812 | SUSAN MOSES MBATTA | Self | 300 | 0.00 |
| 553218 | ANNA IZACK SHOO | Self | 300 | 0.00 |
| 553219 | SUSAN DANIEL NASSORO | Self | 300 | 0.00 |
| 541282 | LEAH JOSEPH MBUJA | Self | 300 | 0.00 |
| 151926 | AHMAD JUMA LAIZER | Self | 300 | 0.00 |
| 232769 | OMAR HASSAN ARABA | Self | 250 | 0.00 |
| 546317 | SHABANI SAID MAPUNDA | Proxy | 250 | 0.00 |
| 501182 | JUMA MOHAMED NGAHAWA | Self | 250 | 0.00 |
| 546320 | PASCHAL MIHAMBO SHIJA | Self | 250 | 0.00 |
| 530197 | BAPTIST JOACHIM NDUNGURU | Proxy | 250 | 0.00 |
| 484769 | LEVINA NGONYANI CHRISTIAN | Self | 250 | 0.00 |
| 546319 | PASCHAL MIHAMBO SHIJA | Self | 250 | 0.00 |
| 546567 | FESTO NGOZI NDALEMYE | Self | 250 | 0.00 |
| 553225 | MOHAMED YUSUPH GALASI | Proxy | 200 | 0.00 |
| 546420 | SHAMILA HAFIDHI SALUM | Proxy | 200 | 0.00 |
| 546624 | SEIF ALLY MASSIMBA | Proxy | 200 | 0.00 |
| 546664 | SEVERINE ROBERT NJAU | Proxy | 200 | 0.00 |
| 546312 | RAPHEL J M CHAMI | Self | 200 | 0.00 |
| 488630 | HILDA BETHUEL UHAGILE | Self | 200 | 0.00 |
| 49883 | FLAVIAN MUSIMU TUNIGA | Proxy | 200 | 0.00 |
| 546650 | BEVIN HEGUYE GASHUMULOLI | Proxy | 200 | 0.00 |
| 546793 | DONALD NZAGA WARIOBA | Self | 150 | 0.00 |
| 234222 | RICHARD THEODOR LIVIGHA | Self | 150 | 0.00 |
| 546619 | HUSSEIN MWAPULLAH | Self | 120 | 0.00 |
| 531300 | PRIMITIVA COSMAS MGAYA | Self | 120 | 0.00 |
| 37590 | PERFEKTUS JOSEPH URIO | Self | 103 | 0.00 |
| 260267 | THEODOSIA A BINAMUNGU | Proxy | 100 | 0.00 |
| 235669 | CLAUDI COSMAS MFUNGO | Self | 100 | 0.00 |
| 131047 | LAMECK MPIRA KUSANYA | Self | 100 | 0.00 |
| 546339 | SALHA YUSUPH KALEMA | Self | 100 | 0.00 |
| 546256 | FRANCIS BENEDICT MWITA | Self | 100 | 0.00 |
| 543438 | REHEMA HUSSEIN KAHABI | Self | 100 | 0.00 |
| 546235 | NICKO MWADUPA HENRY | Self | 100 | 0.00 |
| 546291 | MERISIANA FRANCIS MADUCHE | Proxy | 100 | 0.00 |
| 546363 | GODFREY MEITAMEI MOLLEL | Proxy | 100 | 0.00 |
| 546370 | JACOBO ANAEL KIMARO | Proxy | 100 | 0.00 |
| 546517 | IMAN GODFREY STEPHEN | Self | 100 | 0.00 |
| 546369 | PILLY FADHILI MWESA | Proxy | 100 | 0.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 513731 | PHILIP SADICK MCHAU | Self | 100 | 0.00 |
| 546272 | MUMIN NASSORO MPENDEKELAKI | Proxy | 100 | 0.00 |
| 546463 | DENIS DEOGRATIUS MZUNGU | Self | 100 | 0.00 |
| 527521 | MAJALIWA SHABANI WANYAMALE | Self | 100 | 0.00 |
| 546244 | ANITHA JONATHAN WAINDI | Proxy | 100 | 0.00 |
| 253203 | JOSEPH KIMARIO PHILEMO | Self | 100 | 0.00 |
| 546518 | DICKSON MHORO | Self | 100 | 0.00 |
| 546275 | EMMANUEL E. ISHASI | Proxy | 100 | 0.00 |
| 546516 | GODLISTEN CHARLES LWAMBATI | Self | 100 | 0.00 |
| 546529 | BARNABAS ANDREW KABONA | Proxy | 100 | 0.00 |
| 546483 | LYDIA SOSTHENES CHINGORYA | Self | 100 | 0.00 |
| 546612 | SALIM ABDULMALIKI IBRAHIM | Self | 100 | 0.00 |
| 546647 | JACKSON KASSIM MWANTAJI | Proxy | 100 | 0.00 |
| 121195 | EDGAR LUTAINULWA KAHABWA | Self | 70 | 0.00 |
| 999999 | AHMED NGANYA | Non-Shareholder | 0 | - |
| 999999 | ASHA ATHUMANI MZIGE | Non-Shareholder | 0 | - |
| 999999 | OCTAVIAN MSHIU | Non-Shareholder | 0 | - |

## YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA KUMI NA TATU ULIOFANYIKA TAREHE 30 NOVEMBA 2018

| Kumb. | Maelezo Mafupi | Azimio | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 13.15.1 | Taarifa ya Wakurungezi | Mkutano Mkuu uliazimia kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2017. | Taarifa zilipokelewa |
| 13.15.2 | Malipo ya Gawio | Kampuni ilipe Gawio la Shilingi 2.54 kwa kila his moja | Azimio limetekelezwa kwa wanahisa ambao taarifa zao katika Daftari la Wanahisa zimekamilika Juhudi zinaendelea kupata tarifa za wanahisa waliobaki iliwaweze kulipwa gawio lao. |
| 13,15.3 | Malipo ya Wakurugenzi wa Bodi | Wajumbe wa Bodi walipwe kiasi cha Shilingi 4,000,000 kila Mjumbe wa Bodi. | Azimio limetekelezwa. |
| 13.15.4 | Uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu | CROWE Tanzania ateuliwe kuwa Mkaguzi wa Mahesabu kwa mwaka wa fedha 2018 na kwamba malipo yake yawe Shilingi 16,402,000 | Azimio limetekelezwa. |
| 13.16 | Madai ya Dkt. Gideon H. Kaunda dhidi ya Kampuni. | Wajumbe walizingatia Taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa 13. | Baada ya uamuzi wa Mahakama Kuu (Kitengo cha Biashara) ambao ulitengua Tuzo iliyokuwa imetolewa na Jopo la Wasuluhishi, Dkt. Kaunda alikata rufaa Mahakama ya Rufaa na Kampuni kwa kupitia Mwanasheria wake imewasilisha pingamizi. Uamuzi wa Mahakama ya Rufaa itakapokelewa Wajumbe mtafahamishwa. |

Bodi ya Wakurugenzi

DONDOO NA. 14/5/2019

# TAARIFA YA MWENYEKITI

## 1. Utangulizi

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi na kwa niaba yangu binafsi, ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya utendaji kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018. Katika utendaji, Kampuni ilipata changamoto ndogo ndogo ikiwa ni pamoja na ongezeko la gharama za uendeshaji wa Kampuni, kushuka thamani ya hisa katika Soko la Hisa ikiwa ni pamoja na baadhi ya Makampuni ambayo Kampuni imewekeza hisa kutofanya vizuri. Pamoja na Changamoto hizo, bado Kampuni imeendelea kufanya vizuri. Mwisho napenda kuwajulisha wahahisa kuwa Hisa za Kampuni ziliorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) tarehe16 Machi, 2018.

## 2. Matokeo ya Utendaji

Kwa mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018, faida kabla ya kodi ilipungua kwa asilimia 44 na kufikia Shilingi 195.78 milioni ukilinganisha na mwaka 2017 kutokana na kupungua kwa mapato ya gawio kutoka makampuni ambayo Kampuni imewekeza na pia kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa Kampuni. Hata hivyo, faida baada ya kodi iliongezeka kwa asilimia 49 na kufikia Shilingi 366.57 milioni kutokana na kutambua ongezeko la kodi (Corporate tax) lililokuwa linalipwa kimakosa kutokana na magawio tuliyokuwa tunapokea kutoka kwenye Makampuni ambayo Kampuni imewekeza. Kwa Mwaka wa fedha 2018, Kampuni pia ilipunguza asilimia 20 ya uwekezaji kwenye Hisa (sawa na shilingi bilioni 4.3 ) na kuwekeza kwenye Amana za Serikali (Government Bonds).Hii imechangia kuongezeka kwa faida ya Kampuni kutokana na pato la riba kutoka kwenye Amana hizo.

Kwa mwaka 2018, thamani ya uwekezaji wa Kampuni kwenye Hisa ilishuka kwa Shilingi bilioni 2.03 kutokana na kushuka kwa bei za Hisa za makampuni yaliyoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ukilinganisha na mwaka 2017 ambapo thamani ya uwekezaji wa Kampuni kwenye Hisa iliongezeka kwa Shilingi bilioni 2.73.

Bodi inachukukua hatua Madhubuti kuboresha ufanisi wa Kampuni kwa kupunguza gharama za uendeshaji bila kuathiri utendaji pamoja na uwekezaji makini wenye lengo la kupanua wigo na kuongeza vyanzo mbalimbali vya mapato.

## 3. Gawio

Sera ya Kampuni kuhusu Gawio ni kutoa asilimia hamsini (50%) ya faida inayopatikana baada ya kutenga fungu la kodi kwa wanahisa wake kama gawio baada ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu. Faida inayobaki kwenye Kampuni, inawekezwa ili kukuza mtaji wa Kampuni.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2018, Bodi inapendekeza gawio la Shilingi 2.54 kwa hisa moja ambayo ni sawa na gawio la mwaka 2017. Hili litalipwa baada ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne.

## 4. Matarajio ya Baadaye

Kampuni inategemea kupunguza uwekezaji katika Hisa za makampuni  na kuwekeza maeneo mengine kama hati fungani (Government Bonds),  Majengo, kuagiza na kuuza bidhaa nje ya nchi, Huduma za Bima, na maeneo mengine katika Sekta ya Fedha.

Matarajio ya juhudi hizi ni kuongezeka kwa faida na kuwa na uhakika wa mapato kuliko kutegemea uwekezaji katika hisa pekee ambapo kwa sasa faida yake haitabiriki kulingana na hali halisi ya uwekezaji kwa sasa.

## 5. Shukrani

Mwisho, kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wetu wote ambao wamechangia kwa namna moja au nyingine Kampuni kufikia hapa. Pia, napenda kuwashukuru Menejimenti kwa kujitoa kwao katika kuiendeleza Kampuni. Na mwisho kabisa, napenda kuwahakikishia wanahisa wetu wote kuwa Kampuni itaendelea kufanya vizuri.

__________________________

Ndg. Fortunatus M. Magambo
**Mwenyekiti wa Bodi**
Tarehe: 30 Aprili, 2019

# TAARIFA YA WAKURUGENZI

**1. Utangulizi**

Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Kampuni kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2018.

**1. Uanzishwaji wa Kampuni**

Kampuni ilianzishwa na Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Tanzania (TCCIA) tarehe 9 Novemba, 1999 kulingana na Sheria ya makampuni ya mwaka 2002. Kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wake, Kampuni haikuweza kuanza shughuli za biashara mara moja na badala yake ilianza Oktoba, 2005. Ili kuendana na sheria ya Makampuni ya mwaka 2002, mnamo tarehe 16 Mei, 2016 Kampuni ilibadilisha jina kutoka TCCIA Investment Company Limited na kuwa TCCIA Investment Public Limited Company.

**2. Biashara ya Kampuni**

Biashara ya Kampuni ilikuwa ni kuwekeza katika Hisa za makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa na Hati fungani. Mpaka sasa hakuna kilichobadilika katika hilo.

**3. Matokeo ya Shughuli za Kampuni**

Taarifa ya mahesabu ya Kampuni inaandaliwa kulinga na matakwa ya Sheria ya Kimataifa ya uandaaji wa Taarifa ya Mahesabu (IFRS) pamoja na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Sera hii ndio inayotumika pia katika kuandaa Mahesabu ya Kampuni yetu.
Kwa mwaka wa fedha wa 2018, mapato ya Kampuni yalipungua kwa asilimia 7.4 na kufikia Shilingi bilioni 1.32 ikilinganishwa na mwaka 2017. Hii ilitokana na kupungua kwa mapato ya gawio kutoka kwenye Makampuni ambayo Kampuni imewekeza. Hata hivyo mapato yatokanayo na riba (interest income) yaliongezeka kwa asilimia 102 na kufikia shilingi 425.69 milioni. Hii ilitokana na uamuzi wa Bodi wa kuuza sehemu ya uwekezaji katika Hisa na fedha iliyopatikana ikawekezwa katika hati fungani (Gorvernment Bonds). Kwa upande mwingine gharama za uendeshaji wa Kampuni ziliongezeka kwa asilimia 4.72 na kufikia Shilingi bilioni 1.13.
Vile vile kwa mwaka 2018, mtaji wa Kampuni ulipungua kwa Shilingi bilioni 2.03 ukilinganisha na ongezeko la Shilingi bilioni 2.73 mwaka 2017. Hii iilitokana na kupungua kwa ongezeko la thamani ya Hisa kwa makampuni yalioyoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).
Taarifa zaidi imeonyeshwa kwenye Taarifa ya Mahesabu.

**4. Maono ya Kampuni**

Mpango wa Kampuni ni kuwawezesha wahahisa wake kumiliki uchumi na kujiendesha wenyewe. Hii itawezekana kwa kuwekeza katika vyanzo mbalimbali vitakavyoiingizia Kampuni kipato.

**5. Dhima ya Kampuni**

Dhima ya Kampuni ni kuwawezesha wanahisa wake kufanya uwekezaji wa pamoja. Kampuni inatoa huduma bora kwa mtu mmoja mmoja, mashirika na vikundi mbalimbali kupitia wafanyakazi wake wenye sifa stahiki na wenye uwezo wa kutatua matatizo ya wadau wake.

**6. Ufanyaji Kazi wa Kampuni**

Kampuni inafanya kazi kwa ushirikiano, ufanisi, kujitoa, uadilifu na uwajibikaji kwa wanahisa, wadau wa Kampuni na jamii kwa ujumla.

**7. Malengo ya Kampuni**

Malengo ya Kampuni ni :

- Kukuza na kuimarisha mtaji wake.
- Kuhakikisha Kampuni inapata faida;
- Kuongeza mtaji wa Kampuni na kuongeza thamani ya hisa ya Kampuni kupitia maamuzi ya uwekezaji wenye tija.

**8. Shughuli Kuu ya Kampuni**

Shughuli kuu ya Kampuni ni kusimamia uwekezaji, hasa katika hisa za makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa yanayotengeneza faida, hati fungani na kujenga maghala katika maeneo mazuri ya biashara. Kampuni inawahimiza wanahisa wake kujenga utamaduni wa kuwekeza kwa njia ya hisa.

**9. Mwenendo wa Kampuni.**

Taarifa ya Mahesabu imeandaliwa kulingana na sera ya mahesabu inayotoa picha ya mwenendo wa Kampuni. Msingi huu unazingatia kuwa fedha zitakazopatikana zitasaidia Kampuni kujiendesha na kufadhili shughuli za baadaye na kutambua mali na ufanisi wa madeni, majukumu na ahadi zitakazotokea katika mwenendo wa kawaida kibiashara.

**10. Matukio baada ya kutolewa kwa Taarifa ya Mahesabu**

Wakurugenzi hawajapata taarifa ya jambo lolote lililotokea baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha wa 2018 ambalo linaweza kuathiri Taarifa hii ya Mahesabu.

**11. Mtaji wa Kampuni**

Kwa mwaka 2018, mtaji wa Kampuni uliongezeka kwa silingi millioni 37 na kufikia shilingi 1,459 millioni ukiondoa mtaji ambao Kampuni ilianza nao wa Shilingi 1,421.85 millioni kutokana na mauzo ya Hisa 1,865,260 zenye thamani ya Shilingi 20/- kila moja kwa Shilingi TZS 400/- kila moja.

## 12. Wanahisa wa Kampuni

| | | |
|---|---|---|
| Idadi ya wanahisa kwa mwaka 2018 ilikuwa 3,426. | | |
| Majina ya wanahisa yameorodheshwa hapa chini: | | |
| | **Idadi ya Hisa** | **%** |
| Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) | 28,100,300 | 38.52 |
| Mkombozi Fishing & Maring Transport Ltd | 4,215,000 | 5.78 |
| Abbasi Exports Ltd | 1,686,000 | 2.31 |
| Christopher Mwita Gachuma | 1,405,000 | 1.93 |
| Fayaz Feroz Rashida | 1,236,400 | 1.69 |
| Nimrod Elireheemah Mkono | 1,123,975 | 1.54 |
| Other shareholders (holding less than 1.5%) | 35,190,985 | 48.23 |
| | **72,957,660** | **100.00** |

### 13. Gawio

Sera ya kampuni kuhusu gawio ni kulipa asilimia 50 ya faida inayokuwa imepatikana baada ya kutenga fungu la kodi. Hata hivyo kwa mwaka 2018, Bodi inapendekeza kulipa Shilingi 2.54 kwa hisa moja ambayo ni sawa na Shilingi milioni 185.

### 14. Bodi ya Wakurugenzi

Wakurugenzi wa Kampuni kwa mwaka wa fedha wa 2018 ni hawa wafuatao:

| **Jina la Mkurugenzi** | **Nafasi** | **Taifa** | **Kuchaguliwa/Kustaafu** |
|---|---|---|---|
| Ndg. Fortunatus M. Magambo | Mwenyekiti | Mtanzania | Alichaguliwa, Novemba 30, 2018, |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | Mjumbe | Mtanzania | Alichaguliwa, Novemba 30, 2018 |
| Ndg. Peter William Kifunguomali | Mjumbe | Mtanzania | Alichaguliwa,November 30, 2018 |
| Ndg. Joseph Matanga Kahungwa | Mjumbe | Mtanzania | Alichaguliwa, November 30, 2018 |
| Ndg. Magdalene N.E. Mkocha | Mjumbe | Mtanzania | Alichaguliwa,November 30, 2018 |
| Ndg. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | Mtanzania | Alichaguliwa, November 30, 2018 |
| Ndg. Octavian Mshiu | Mjumbe | Mtanzania | Alichaguliwa,November 30, 2018 |
| Mhandisi. Aloys J. Mwamanga | Mwenyekiti | Mtanzania | Alistaafu,November 30, 2018 |
| Ndg. Arphaxad G. A. Masambu | Mjumbe | Mtanzania | Alistaafu,November 30, 2018 |
| Dkt. Gideon H. Kaunda | Mjumbe | Mtanzania | Alistaafu,November 30, 2018 |
| Ndg. Ndibalema J. Mayanja | Mjumbe | Mtanzania | Alistaafu,November 30, 2018 |
| Ndg. Nathaniel R. Mbwambo | Mjumbe | Mtanzania | Alistaafu,November 30, 2018 |
| Ndg. Julius M. Kaijage | Mjumbe | Mtanzania | Alistaafu,November 30, 2018 |

**Ndg. Ndibalema John Mayanja**, ambaye alikuwa anawakilisha TCCIA na matawi yake kwa nafasi ya Urais, alifariki Juni, 2018 na nafasi yake katika Bodi ikabaki wazi hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2018 ilipojazwa na Ndg. Octavian E. Mshiu

**15. Idadi ya Hisa za kila Mkurugenzi kwenye Kampuni:**

| Jina la Mkurugenzi | Idadi ya Hisa Anazomiliki |
|---|---|
| Prof. Lucian A. Msambichaka | 487,580 |
| Ndg. Peter William Kifunguomali / Ndg. Fortunatus M. Magambo** | 28,100,300 |
| Ndg. Joseph Matanga Kahungwa | 40,600 |
| Ndg. Magdalene N.E. Mkocha | 102,363 |
| Ndg. Nathan E. Mnyawami | 19,675 |
| Mhandisi. Aloys J. Mwamanga | 231,975 |
| Ndg. Arphaxad G. A. Masambu | 74,625 |
| Ndg. Gideon H. Kaunda | 112,400 |
| Ndg. Ndibalema J. Mayanja** | 830,498 |
| Ndg. Nathaniel R. Mbwambo | 303,462 |
| Ndg. Julius M. Kaijage | 18,113 |
| | 30,321,591 |

****Ndg. Ndibalema John Mayanja** alihudumu kwenye Bodi mwaka 2018 kama rais wa TCCIA na aliiwakilisha TCCIA Makao Makuu na matawi yake ambao wanamiliki jumla ya hisa 830,213. Hata hivyo alifariki Juni, 2018, na nafasi yake kubaki wazi hadi 30 Novemba, 2018 ilipojazwa na Ndg. Octavian E. Mshiu.
**Ndg. Peter William Kifunguomali / Ndg. Fortunatus M. Magambo wanawakilisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii LAPF wanaomiliki jumla ya hisa 28,100,300.

**16. Katibu wa Bodi**

Katibu wa Kampuni ni Ndg Donald Jimogi Kamori.
Anuani ya Posta:S. L. P 72678, Dar Es Salaam

**17. Majukumu ya Bodi**

Pamoja na majukumu mengine ya kusimamia shughuli za Kampuni, Bodi ina majukumu yafuatayo:-

- Kusimamia zoezi la uorodheshaji wa Hisa za Kampuni katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, ambazo ziliorodheshwa tarehe 16 Machi, 2018.
- Kuandaa Katiba ya Bodi.
- Kuandaa taarifa ya Maendeleo ya Kampuni ya kila robo mwaka.
- Kupitia njia mbalimbali za kupunguza gharama za uendeshaji wa Kampuni ikiwemo kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi, Kuhamisha ofisi kutoka katikati ya mji na kuhamia nje ya mji ambapo gharama za ofisi ni nafuu.
- Kuandaa Mpango Mkakati wa mwaka na Bajeti ya mwaka mzima.
- Kuandaa uchambuzi wa kina wa mpango mkakati wa eneo la Kampuni la kujenga maghala ya kuhifadhia bidhaa mbalimbali lililoko Mtwara na fursa nyingine za kibiashara.

**18. Mipango ya Baadaye**

Kama mjuavyo Kampuni iliuza hisa zake mwanzoni mwa mwaka 2017 kuanzia tarehe 1 Februari hadi

tarehe 14 Machi. Lengo ilikuwa ni kukusanya Shilingi bilioni 45. Hii ingesaidia kukuza mtaji wa Kampuni na kupanua wigo wa biashara. Hata hivyo kutokana na hali ya biashaya ya hisa kutokuwa nzuri, zoezi hili halikufanikiwa kwa kiasi kikubwa. Kampuni ilifanikiwa kukusanya Shilingi 746,104,600 tu.

Hata hivyo baada ya kufungwa kwa zoezi la uuzwaji wa hisa za Kampuni, Bodi ilitakafakari upya kwa kushauriana na Mshauri wa Kiongozi kuhusu kuorodhesha hisa za Kampuni kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ukilinganisha na hali halisi ya kiuchumi. Kufikia mwishoni mwaka mwaka 2017, Bodi iliamua kuomba kuorodhesha hisa za kampuni kwenye robo mwaka ya kwanza ya mwaka 2018. Hisa za Kampuni ziliorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) tarehe16 Machi, 2018.
Mwanzoni mwa mwaka 2018, Wakurugenzi waliamua kupanua wigo wa uwekezaji wa Kampuni kwa kuwekeza kwenye maeneo mengine ambayo ilikuwa bado. Toka Kampuni ilipoanza biashara mwaka 2005, zaidi ya asilimia 95 ya uwekezaji ilikuwa ni kwenye hisa za makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam. Bodi iliamua kuwekeza kwenye Hati fungani (Government Bonds). Hata hivyo Bodi inaamini uwekezaji huu utailetea Kampuni faida kubwa kwa wakati ambayo hisa zitakuwa hazifanyi vizuri sokoni kama ilivyo sasa.

Kama mlivyojulishwa kwenye Mkutano Mkuu mwaka 2017, Bodi ilifanikiwa kupata hati ya umiliki wa eneo la Kampuni lililoko Mtwara. Bodi pia imeshafanya uchambuzi wa mpango mkakati kwa ajili ya kujenga maghala ya kuhifanyia bidhaa mbalimbali. Kwa mwaka 2019, Bodi itaendelea kufuatilia maendeleo ya hali ya uwekezaji Mtwara na wakati itakapoimarika Bodi itaanza utekelezaji wa mradi. Hata hivyo, juhudi Madhubuti zinafanyika kutafuta maeneo sehemu mbalimbali kwa ajili ya kujenga maghala. Kwa sasa Bodi inalenga kufuatilia maeneo katika miji ya Dodoma na Tanga.

Mwisho, Bodi inatafuta fursa nyingine za kibiashara ikiwemo kuuza na kununua bidhaa ndani na nje ya nchi, huduma za bima, na biashara mbalimbali katika sekta ya fedha kama vile maduka ya kubadilisha fedha (Bureau de Change shops) na huduma za kifedha za kielektoniki. Hata hivyo kabla ya kuanza kwa hizi biashara, bodi itafanya utafiti wa mpango mkakati kwa kila biashara ambayo itaipa Kampuni faida na pia kama Kampuni itakuwa na mtaji wa kutosha na wataalam eneo husika.

**19. Utawala Bora**

Sheria ya Kampuni inasema, wajumbe wa Bodi wanatakiwa kuwa saba (7) na wasizidi kumi na mbili (12). Mwaka 2018, Bodi ilikuwa na wajumbe kumi na moja (11). Hakuna mjumbe wa Bodi ambaye ni Mfanyakazi wa Kampuni. Bodi ina jukumu la kusimamia Kampuni pamoja na mambo mengine ikiwa ni pamoja na kudhibiti athari zinazoweza kuathiri shughuli za kampuni, kufuatilia kwa karibu na kufanya maamuzi ya maeneo ya uwekezaji. Bodi ina wajibu wa kuhakikisha sheria na taratibu zinafuatwa kwa kuzingatia kanuni za utawala bora.

Kwa mwaka 2018, Bodi ilifanya vikao kumi (10), ambapo vikao sita (6) vilikuwa vya kawaida na vikao maalum vinne kwa ajili ya kupitisha mambo muhimu ambayo yalihitaji umakini wa Bodi. Bodi inamwelekeza Afisa Mtendaji Mkuu kusimamia shughuli za kila siku za Kampuni akisaidiwa na wafanyakazi walio chini yake. Wafanyakazi pia wanahudhuria vikao vya Bodi na kuonyesha ufanisi katika Shughuli za Kampuni. Vikao maalum ni pamoja na kujadili na kupitisha mpango mkakati wa

mwaka na bajeti ya mwaka mzima, Mahesabu yaliyokaguliwa na zoezi la uorodheshwaji wa hisa za Kampuni ambalo lilifanyika tarehe 16 Machi, 2018.
Wajumbe waliohudhuria vikao mwaka 2018 na idadi ya vikao walivyohudhuria:

| **Jina** | **Nafasi** | **Idadi ya Vikao** | **Idadi ya vikao alivyohudhuria** |
|---|---|---|---|
| Ndg. Aloys J. Mwamanga | Mwenyekiti | 10 | 3 |
| Ndg. Peter W. Kifunguomali | Mjumbe | 10 | 8 |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | Mjumbe | 10 | 10 |
| Ndg. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 10 | 10 |
| Ndg. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | 10 | 10 |
| Ndg. Julius M. Kaijage | Mjumbe | 10 | 9 |
| Ndg. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 10 | 8 |
| Ndg. Arphaxad G. A. Masambu | Mjumbe | 10 | 8 |
| Dkt. Gideon H. Kaunda | Mjumbe | 10 | 9 |
| Ndg. Ndibalema J. Mayanja | Mjumbe | 10 | 1 |
| Ndg. Nathaniel R. Mbwambo | Mjumbe | 10 | 8 |
| | | 110 | 84 |

Bodi inatambua na kufuata kanuni za utawala bora. Ili kuhakikisha Bodi inatimiza majukumu yake vizuri, kwa mwaka 2018, Bodi ilikuwa na Kamati mbili ambazo ni:

- Kamati ya Uwekezaji ambayo ilikuwa na wajumbe wanne.
- Kamati ya Ukaguzi na Athari za Kampuni ambayo ilikuwa na wajumbe watatu

**Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji walikuwa ni:**

1. Prof. Lucian A. Msambichaka - Mwenyekiti.
2. Ndg. Arphaxad G.A Masambu - Mjumbe.
3. Ndg. Nathan E. Mnyawami - Mjumbe.
4. Dkt. Gideon H. Kaunda - Mjumbe.

Kwa mwaka 2018, Kamati ya Uwekezaji ilikutana mara sita kujadili taarifa ya kila robo ya mwaka, upembuzi wa mpango mkakati wa kujenga maghala ya kuhifanyia bidhaa mbalimbali Mtwara na mpango mkakati wa mwaka pamoja na bajeti kabla ya kuiwasilisha kwenye Bodi kwa maamuzi.
Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi na Athari za kampuni ni:-

1. Ndg. Joseph M. Kahungwa - Mwenyekiti.
2. Ndg. Peter W. Kifunguomali - Mjumbe.
3. Ndg. Magdalene N.E. Mkocha - Mjumbe.

Kwa mwaka 2018, Kamati ilikutana mara sita kujadili taarifa ya ukaguzi wa ndani ya kila robo mwaka inayoandaliwa na Mkaguzi wa ndani na kutoa mapendekezo yao na kujadili taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa ya mwaka inayoandaliwa na Mkaguzi wa nje.

**20. Athari zinazoweza kujitokeza na Namna ya kudhibiti**

Bodi inakubali jukumu la mwisho la usimamizi wa athari na mifumo ya udhibiti wa ndani wa

Kampuni. Ni kazi ya Menejimenti kuhakikisha mfumo wa ndani wa kifedha pamoja na uendeshaji wa Kampuni inaendelezwa na kudumishwa ili kuhakikisha misingi iliyowekwa inadumishwa na ya uhakika wa:

- Ufanisi wa shughuli za Kampuni
- Kulinda mali za Kampuni;
- Kusimania sheria na kanuni zilizowekwa;
- Kuwepo kwa kumbukumbu za mahesabu pale zinapohitajika;
- Kuhakikisha shughuli za Kampuni zinaendelea kwa wakati wote;
- Kuwajibika kwa wadau wa Kampuni.

Ufanisi wa mfumo wowote wa ndani unategemea na kuzingatia sheria zilizowekwa. Daima kuna athari zitakazojitokeza endapo wafanyakazi hawatazingatia sheria zilizowekwa. Ingawa hakuna mfumo wa udhibiti wa ndani unaweza kutoa uhakika kamili dhidi ya taarifa au mapungufu au hasara, mfumo wa kampuni umeundwa kudhibiti na kuhakikisha taratibu zilizopo zinafuatwa kwa ufanisi.

Katika mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2018, Bodi ilipima mifumo ya udhibiti wa ndani na kujiridhisha kuwa una vigezo vinavyokubaliwa.

**21. Ustawi wa Wafanyakazi**

Uhusiano kati ya wafanyakazi wa ngazi ya chini na ngazi ya juu uliendelea kuwa mzuri kwa mwaka 2018. Hapakuwa na malalamiko yasiyotatulika kutoka kwa uongozi wa juu wa Kampuni.

Kampuni inatoa haki sawa kwa wafanyakazi wote. Inatoa fursa sawa ya ajira na kuhakikisha kwamba mtu bora zaidi anayepatikana anapewa nafasi bila ubaguzi wa aina yoyote na bila kujali jinsia, hali ya ndoa, makabila, dini na ulemavu ambao hauathiri uwezo wa kufanya kazi.

Jumla ya wafanyakazi wa Kampuni kwa mwaka 2018 walikuwa watano (5) (2017: 5).

**22. Misaada kwenye Siasa na Jamii kiujumla**

Kwa mwaka 2018, Kampuni haijatoa msaada wowote wa kisiasa au kusaidia jamii.

**23. Wakaguzi wa Mahesabu**

Wakaguzi wa Mahesabu ya Kampuni, CROWE Tanzania, wameonyesha nia yao ya kuendelea kukagua mahesabu ya Kampuni na wako tayari kuteuliwa tena. Azimio la kupendekezwa kuteuliwa upya kama Wakaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka 2019 litawasilishwa.

Taarifa ya mahesabu imeonyeshwa kwenye ukurasa wa 19 na 45, ambayo imeandaliwa na kutoa mwelekeo mzuri wa Kampuni na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi na kusainiwa kwa niaba yao na:

Ndg. Fortunatus M. Magambo
**Mwenyekiti wa Bodi**
Tarehe: 30 Aprili, 2019

Ndg. Joseph M. Kahungwa
**Mkurugenzi**
Tarehe: 30 Aprili, 2019

# WAJIBU WA WAKURUGENZI

Kulingana na sheria ya makampuni ya mwaka 2002, Bodi ina wajibu wa kuandaa taarifa ya mahesabu ya Kampuni na taarifa zingine zinazohusiana na hizo ambazo zimeunganishwa kwenye taarifa hii. Wakurugenzi wana jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa ya fedha inatoa picha halisi ya Kampuni kila mwisho wa mwaka wa fedha na matokeo ya shughuli za Kampuni mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi ambacho kinakamalizika, kulingana na Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Taarifa za Fedha. Wakaguzi wa nje wanatakiwa kutoa maoni ya kujitegemea kwenye taarifa za fedha.

Wakurugenzi wana wajibu wa kusimamia na kudhibiti mfumo wa ndani wa kifedha uliowekwa na Kampuni na kuweka umuhimu mkubwa katika kudumisha mazingira mazuri ya udhibiti. Ili kuwawezesha wakurugenzi kufikia malengo haya, wanatakiwa kuweka mikakati ya kupunguza au kuondoa kabisa hasara kwa gharama yoyote. Hii inajumuisha mpangilio wa majukumu, na mgawanyo wa kazi. Wafanyakazi wote wanapaswa kudumisha kiwango cha juu cha maadili ili kuhakikisha kazi zinafanyika kwa usahihi na kuondoa mazingiza yoyote yanayoweza kuisababishia Kampuni hasara.

Ni vizuri kutambua, kutathmini, kusimamia na kufuatilia aina zote za hatari katika kampuni. Athari katika uendeshaji wa Shughuli za Kampuni haiwezi kuondolewa kabisa bali inaweza kupunguzwa kwa kuhakikisha kwamba miundombinu sahihi, udhibiti, mifumo na tabia ya kimaadili hutumiwa na kusimamiwa ndani ya taratibu zilizowekwa.

Maoni ya Wakurugenzi kutokana na maelezo waliyopokea kutoka kwa Menejimenti, ni kwamba mfumo wa udhibiti wa ndani unatoa uhakika kwamba, taarifa ya fedha zinaweza kutegemewa kwa ajili ya maandalizi ya taarifa ya mahesabu. Hata hivyo, mfumo wowote wa udhibiti wa kifedha wa ndani unaweza kutoa tu picha lakini sio uhakika dhidi ya kupotea au hasara iliyotokea.

Wakurugenzi wamepitia makisio ya utayarishaji wa Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka huu unaoishia Desemba 31, 2019 na kwa mujibu wa tathmini hii na hali ya kifedha ya Kampuni kwa sasa, unaridhisha kuwa Kampuni ina rasilimali za kutosha na itaendelea kufanya vizuri.

Wakaguzi wa nje wanajibika kukagua na kutoa taarifa ya mahesabu ya Kampuni. Taarifa ya mahesabu ya kampuni iliyokaguliwa imewasilishwa kwenye ukurasa wa 16 hadi 15.
Taarifa za Mahesabu imeambatanishwa kwenye ukurasa wa 19 hadi 45, ambazo zimeandaliwa na kuidhinishwa na bodi ya wakurugenzi na kusainiwa na:

| | |
|---|---|
| ....................................... | ....................................... |
| Ndg. Fortunatus M. Magambo | Ndg. Joseph M. Kahungwa |
| **Mwenyekiti wa Bodi** | **Mkurugenzi** |
| Tarehe: 30 Aprili, 2019 | Tarehe: 30 Aprili, 2019 |

DONDOO NA.14/6/ 2019

KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA MAHESABU YA KAMPUNI
YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA
TAREHE 31 DESEMBA, 2018.

DONDOO NA.14/7/2019

## KUTANGAZA GAWIO

Sera ya Kampuni kuhusu Gawio ni kutangaza na kulipa gawio ambalo ni sawa na asilimia 50 ya faida inayopatikana baada ya kutenga fungu la Kodi. Hii ina maana kwamba kwa kuzingatia faida iliyopatikana kwa mwaka 2018 baada ya kutenga fungu la Kodi, kiasi kinachopaswa kutengwa kwa ajili ya malipo ya gawio ni Shilingi 185.0 milioni. Kiasi hiki ni sawa na Shilingi 2.54 kwa hisa moja. Kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kiasi cha faida kinachobaki kitatumika kuimarisha mtaji wa Kampuni.

Vilevile, Bodi inapendekeza kuwa kama Mkutano Mkuu utaridhia pendekezo hili, malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike siku tisini (90) baada ya kupitisha azimio hili. Kwa wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao.

Mkutano Mkuu unaombwa kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo hili.

**Bodi ya Wakurugenzi**

DONDOO NA.14/8/ 2019

## UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2019

Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2018, Mahesabu ya Kampuni yalikaguliwa na Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu na Ushauri ya CROWE Tanzania Limited. Hadi sasa Bodi imeridhika na kazi ambayo ilifanywa na Kampuni hii kwa mwaka 2018. Aidha Kampuni hiyo imeonyesha nia ya kuendelea kukagua Mahesabu ya Kampuni yetu kama watateuliwa tena.

Bodi inapendekeza kuwa CROWE Tanzania Limited wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampani kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2019. Ada ya Ukaguzi inayopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 17,525,000 pamoja na VAT. Ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

Mwisho Bodi inapendekeza kuwa Mkutano Mkuu ujadili na kuidhinisha pendekezo la Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania Limited waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Desemba 31, 2019.

Pamoja na kuidhinisha Shilingi 17,525,000 Kama gharama za malipo ya ukaguzi wa mehesabu ya Kampuni.

**Bodi ya Wakurugenzi**

DONDOO NA.14/9/2019

## PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Malipo ya Wajumbe wa Bodi, [Directors fees] yameainishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 [i] kinaeleza kuwa: "The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in General Meeting".

Malipo haya huwa yanawekwa kwenye Bajeti ya Kampuni kila mwaka. Malipo ya Wajumbe yanatokana na ukweli kuwa Wajumbe wa Bodi hutumia muda mwingi kusimamia shughuli za Kampuni, badala ya kusimamia shughuli zao binafsi. Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa Bodi ndio wanawajibika kwa Mkutano Mkuu kwa kusimamia shughuli za Kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, pamoja na kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam, utawala bora na ufanisi wa Kampuni. Kwa kifupi chini ya Sheria ya Makampuni, Wajumbe wanawajibika kuhakikisha kuwa wanasimamia vema Kampuni ili wanahisa wasipoteze fedha zao na kwamba mtaji wa Kampuni unakua.

Kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2018, Bodi inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne (Shilingi 4,000,000), kiasi ambacho ni sawa na malipo yaliyoidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2018.

Mwisho, Mkutano Mkuu unaombwa, kupokea, kujadili na kuridhia malipo ya Shilingi milioni nne (Shilingi 4,000,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi.

**Bodi ya Wakurugenzi**

**TCCIA INVESTMENT PLC**
P. O. Box 72678 Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 684 535 545 Fax: 255 – 22 – 2119437
Email: info@tcciainvestment.com, Web site: https://www.tcciainvestment.com